

## SWAHILI

### **Taarifa na Fomu za Ushawishi za Uamuzi wa Wazazi ya Matunzo ya Mwanzo ya Utoto na Utaratibu wa Elimu (ECCE) na Utaratibu wa Jumuiya ya Ruzuku ya Matunzo ya Mtoto (CCS)**

Matunzo ya Mwanzo ya Utoto na Utaratibu wa Elimu (ECCE) hutoa elimu ya bure mwakani kwa watoto kabla hawajaanza elimu ya msingi. Matunzo ya Mwanzo ya Utoto na Utaratibu wa Elimu (ECCE) inatoa pesa za msaada kwa jumuiya si tu kwa manufaa ya huduma ya mtoto, ya kuwawezesha kulipisha pesa zilizopunguzwa za matunzo ya mtoto kwa wasiojiweza na wazazi wanao mapato ya chini. Maelezo ya utaratibu yametolewa katika barua kwa wazazi ambayo wanapaswa kupokea kutoka kwa Huduma ya Matunzo ya Watoto na Fomu ya Azimio ya Mzazi. Mwaka wa Elimu ya bure ya kabla– Shule (ECCE) kwa kawaida itamulika mwaka wa shule ya msingi.

**KUM. Mzazi hawezi kudai msaada kwa niaba ya mtoto ambaye tayari amenufaika, ila tu wamepata ruhusa kwa maandishi kutoka kwa OMCYA. Kama mzazi amepata ruhusa hiyo, wanapaswa kuambatanisha nakala yake kwa fomu ya azimio.**

Ni mzazi moja tu anapaswa kujaza fomu hii. Kama anadai usaidizi wa CCS, lakini ni mzazi moja tu ndiye atakayepokea malipo yaliyohitimu, mzazi huyo anapaswa kujaza fomu. Wazazi wanapaswa kuandika majina yao wenyewe na nambari ya PPS, jina, tarehe ya kuzaliwa na nambari ya PPS ya mtoto wao. Jina la huduma matunzo ya mtoto anayohudhuria na mtindo (wiki 38 au wiki 50) chini ya utaratibu wa ECCE ambayo imechaguliwa (mahali itakapotumika) pia lazima ijazwe. Wazazi wanapaswa kurudisha fomu ya azimio iliyojazwa (iliotiwa saini) kwa huduma ya matunzo ya mtoto inayohudhuriwa kulingana tarehe kama ilivyokubaliwa na huduma. Huduma ya Matunzo ya Mtoto itapeleka taarifa iliyotolewa kwa fomu zilizokamilishwa, kwa ujasiri, kwa Afisi ya Waziri wa Watoto na Mambo ya Vijana (OMCYA), ambayo ni moja wapo ya Idara ya Afya na Watoto. Hii ni ya kuwezesha taarifa iliyotolewa kuthibitishwa na kiwango cha utoaji msaada wa CCS na/au malipo ya kodi ya wa/motto kulipwa kwa huduma.

**Inapaswa kuangaliwa kwamba malipo ya ECCE haiwezi kudaiwa kwa mtoto kwa nyongeza ya fedha za msaada yake chini ya CCS. Hata hivyo, wazazi wanaochagua kunufaika kwa utaratibu wa ECCE kwa mtoto wanaweza kudai msaada chini ya CCS kuanzia Septemba inayofuata.**

**Kuwasaidia wazazi kwa kujaza fomu za azimio zinazohitajika, hapa kuna orodha ya wasaha kwa maswali yanayoulizwa kwa fomu ya azimio:**

Swali kwa Kingereza	Question in English
1. Azimio la Mzazi/Mlezi	1. Declaration by the Parent/Guardian
2. Je jina kamili la familia ni: Jina la kwanza na jina la familia?	2. What is the full family name: first name and surname?

3. Je nambari yako ya PPS ni?	3. What is your PPS number?
4. Je jina la Huduma ya Matunzo ya mtoto ni gani?	4. What is the name of the Childcare Service?
5. Je jina la mtoto wako ni gani kama ilivyoandikwa katika hati rasmi k.m.e cheti chake cha kuzaliwa?	5. What is your child's name as stated in official documents eg his/her birth certificate?
6. Je unatuma ombi la ECCE ( Elimu ya bure ya kabla-shule ya mwakani) au CCS (fedha za masaada za matunzo yako ya mtoto)?	6. Are you applying for the ECCE (free pre-school year) or the CCS (subvention towards your childcare costs)?
7. Nambari ya PPS ya mtoto wako ni ipi?	7. What is your child's PPS number?
8. Je mtoto wako ni kijana (K) au Msichana (M)?	8. Is your child a boy (M) or girl (F)?
9. Je ni shule ipi ya Msingi uliyo peleka mtoto wako?	8. What Primary school have you enrolled your child in?

Taarifa inayotolewa na wazazi kwa fomu ya azimio itapatikana katika ofisi ya Waziri wa Watoto na Mambo ya Vijana (OMCYA) ambayo ni sehemu ya Idara ya Afya na Watoto na itathibitishwa na Idara ya Hifadhi Jamii kabla ya ufadhili utolewe na Serikali kwa Huduma ya Matunzo ya Watoto mahali mtoto wako amesajiliwa.

## Kubadilisha Airishi

Imefadhiliwa na Serikali ya Airishi  
chini ya Mpango wa Ustawi wa Kltifa 2007-2013

